

JINA _____ NAMBA _____ KIDATO _____

IDARA YA LUGHA KIDATO CHA TATU

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

MACHI 2021

MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

- i. Jibu maswali manne pekee.
- ii. Swali la kwanza ni la lazima
- iii. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Tamthilia, Riwaya, na Fasihi Simulizi
- iv. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- v. Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	

	JUMLA 80	
--	-----------------	--

SEHEMU A: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

1. Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa

Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!

Mrithi nini wanangu?
2. Sina ngo'mbe sina mbuzi, sina konde sina buwa
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa

Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa

Mrithi nini wanangu?
3. Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi, mno nikukamuliwa

Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa

Mrithi nini wanangu?
4. Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa

Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa

Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa

Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa

Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa

N'nawana na miliki, hadi nitakapofukiwa

Mrithi nini wanangu?

7. Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongora
Mwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa

Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa

Mrithi nini wanangu?

MASWALI

- (a) **Taja** mambo yoyote mawili ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. (alama 2)
- (b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama 3)
- (c) **Andika** ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
- (d) **Dondoa** mifano miwili miwili ya : (alama 2)
- (i) Inkisari
- (ii) Tabdila
- (e) **Chambua** shairi hili kwa upande wa :
- (i) Dhamira (alama 2)
- (ii) Muundo (alama 4)
- (f) **Eleza maana** ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)
- (i) Mlimwengu kanipoka
- (ii) Sina konde sina buwa.
- (iii) Wingi wa shakawa.

SEHEMU B: TAMTHILIA YA KIGOGO (Pauline Kea)

2. " Wamenimaliza... Wamenigeuka..."

- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
- b) Eleza namna msemaji amemalizwa na kugeukwa?(Alama 4)
- c) Eleza umuhimu wa msemaji. (Alama 4)
- d) Eleza jinsi wahusika wengine walivyomaliziwa katika tamthilia. (Alama 8)

3. (a) Fafanua jinsi mwandishi wa Kigogo alivyofanikisha matumizi ya Majazi. (alama 10)

(b) Ukiukaji haki na uvunjaji sheria ni mambo yaliyokithiri katika jimbo la Sagamoyo. Thibitisha. (alama. 10)

SEHEMU C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K MATEI)

4. Jadili ufaafu wa anwani *Chози la Heri* katika Riwaya. (alama 20)

5. "... mwanaume hufumbika hisia. Machozi ya mwanaume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya Maisha..."

- a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
- b) Tambua mbinu ya lugha kwenye dondoo hili. (alama 2)
- c) Eleza maudhui yanayodhihirishwa na dondoo hili. (alama 2)
- d) Fafanua sifa za msemewa wa dondoo. (alama 12)

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

6.

- a) Taja aina mbili za Fasihi (alama 2)
- b) kwa kutolea hoja nane Tofautisha kati ya Fasihi ulizotaja hapo juu. (alama 8)
- c) (Eleza maana ya Mighani. (alama 2)
- d) Jadili umuhimu wa mighani. (alama 8)

7.

Ewe kilizi

Ulozowe kujificha

Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio

*ya radi ilo juu mbinguni
Jua kesho ni siku ya siku
Siku ya kujua mbichi na mbivu
Kutofautisha jogoo na vipora,
Ngariba taposhika, chake kijembe
Ndipo utakapojua bayani
Ukoo wetu si wa kunguru
Ikiwa hu tayari
Kisu kukidhihaki
Sithubutu kamwe, wanjani kuingia
sije kuniaibisha miye, amiyo na akraba nzima!*

- a) Huu ni wimbo wa aina gani? Toa sababu. (alama 2)
- b) Wimbo huu unaimbwa na nani ? Toa idhibati. (alama 2)
- c) Fafanua sifa nane za huu. (alama 8)
- d) Je, nyimbo za aina hii zina dhima gani kwenye jamii. (alama 8)